**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2008**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Eleza matokeo ya kutozingatia muhtasari katika maandalizi ya mwalimu.
2. Tathmini changamoto zinazoweza kumkumba mwalimu anapotegemea zaidi zana zilizotengenezwa viwandani.
3. Eleza kwa nini ni muhimu kupima wanafunzi mara kwa mara badala ya mwisho wa muhula pekee.
4. Changanua athari za kutozingatia mahitaji ya wanafunzi wenye tabia tofauti wakati wa kujifunza.
5. Eleza namna michezo inavyoweza kuchangia kujenga tabia ya kuthubutu miongoni mwa wanafunzi.
6. Jadili athari za kutokujali usalama wa vifaa vya michezo.
7. Onyesha uhusiano kati ya ubunifu wa mwalimu na ubora wa zana za kufundishia.
8. Eleza umuhimu wa malengo mahsusi katika kufanikisha malengo makuu ya somo.
9. Tathmini nafasi ya misingi ya ufundishaji katika kuondoa changamoto za upungufu wa vifaa vya kujifunzia.
10. Eleza madhara ya kutokufanya maandalizi ya kutosha kabla ya kufundisha somo la Haiba na Michezo.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili katika sehemu hii

11. Eleza kwa kina jinsi maandiko ya mwalimu yanavyoweza kusaidia kuimarisha ujifunzaji wa mwanafunzi.
12. Changanua nafasi ya upimaji na tathmini katika kugundua vipaji vya wanafunzi.
13. Tathmini mchango wa zana za kufundishia katika kuimarisha ushirikiano kati ya wanafunzi na mwalimu.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

14. Eleza vikwazo vinavyoweza kumkumba mwalimu anapopanga maandalio ya somo.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili katika sehemu hii.

15. Jadili changamoto za kutegemea vifaa vya asili pekee katika kufundishia somo la Haiba na Michezo.

16. Eleza nafasi ya misingi ya ufundishaji katika kuimarisha mshikamano wa wanafunzi.

17. Tathmini umuhimu wa kiongozi cha mwalimu katika kuhakikisha usawa wa elimu.

18. Eleza mchango wa somo la Haiba na Michezo katika kumjenga mwanafunzi kiakili na kimwili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org